102/3
KISWAHILI
FASIHI
KARATASI YA TATU
JULAI / AGOSTI 2016
MUDA: 2 ½

# JARIBIO LA MTIHANI WA MWAKA - 2016

**CHETI CHA KUHITIMU MASOMO**

**KIDATO CHA 3**

**KISWAHILI FASIHI**

**KARATASI YA TATU**

**MUDA: 2 ½**

for free past papers visit www.kcsepastpapers.com or call : 0720502479

**MAAGIZO**

1. Jibu maswali **manne** pekee.
2. Swali la kwanza ni la **lazima.**
3. Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani: Riwaya, Hadithi Fupi, Ushairi na Fasihi simulizi.
4. Usijibu maswali **mawili** kutoka sehemu moja.
5. Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
6. Karatasi hii ina kurasa **nne** zilizopigwa chapa.
7. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

**SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI** **(alama 20)**

1. **SWALI LA LAZIMA**

(a) Maghani ni nini? (alama 2)
(b) Fafanua aina zozote **tatu** za maghani. (alama 6)
(c) Eleza sifa za maghani. (alama 6)
(d) Fafanua dhima za maghani katika jamii. (alama 6)

**SEHEMU YA B: TAMTHILIA**
***Timothi Arege: MSTAHIKI MEYA***
***Jibu swali la 2 au 3***

2. Mbinu ya utatu imejikita katika tamthilia ya Mstahiki Meya, jadili. (alama 20)

**AU**

3. Riwaya; Kidagaa Kimemwozea; Ken Walibora.

Jadili namna usaliti umejitokeza katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea ya Ken Walibora. (alama 20)

***Jibu swali la 4 au 5***

4. Hadithi Fupi; Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.

"Usijisumbue nitafika"…alisema kwa roho ya kisebusebu na kijoyo ki papo.

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Ni tamathali gani ya usemi iliyotumika katika dondoo hii. (alama 2)
(c) Eleza changamoto zinazowakumba wasomi kule ughaibuni. (alama 14)

**AU**

5. SHAIRI

**Soma shairi lifuatayo kisha ujibu maswali yote.**

Nami nambe, niwe kama waambao
Niumpambe, uendeze wasoma
Niufumbe, wafumbuwe wawezao.

Kuna mambo, mtoni 'metakabari'
Ajigamba na kujiona hodari
Yuwaambe, wamba aaishi dahari

Meghururi, ghururi za kipumbavu
Afikiri, hutaishwa na nguvu
Tabakuri, hakika ni maangavu

for free past papers visit www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

Akumbuke, siku yake itafika
Roho yake, ajuwe itamtoka
Nguvu zake, kikomche zitafika

Afahamu, mtu hajuwi la kesho
Hatadumu, angatumia vitisho
Maadamu, lenye mwanzo lina mwisho

**MASWALI**

(a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka. (alama 1)

(b) Eleza maudhui yanayojitokeza katika shairi hili. (alama 4)

(c) Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)

(d) Andika ubeti wa 2 kwa lugha ya nathari. (alama 3)

(e) Taja na utoe mifano ya tamathali **mbili** za usemi ambazo zimetumiwa katika shairi hili. (alama 2)

(f) Tambua fumbo lililofumbwa katika shairi hili kama anavyodai mshairi katika ubeti wa kwanza. (alama 2)

(g) Bainisha mifano **miwili** ya uhuru wa mshairi katika shairi hili. (alama 2)

(h) Eleza maana za maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa kwa shairi. (alama 2)
   (i) Dahari
   (ii) Ghururi

for free past papers visit www.freekcsepastpapers.com or call : 0720502479